TAARIFA KWA UMMA YA NDG. LUHAGA JOELSON MPINA KUHUSU UCHAMBUZI WA RIPOTI YA JUMUIYA YA MADOLA KWENYE KIKAO CHA 73 CHA DHARURA CHA MAWAZIRI WA MAMBO YA NJE NA UONGOZI WA KIDEMOKRASIA (CMAG) KILICHOFANYIKA TAREHE 10 JULAI 2026 KUHUSU HALI YA KISIASA NCHINI TANZANIA BAADA YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2025 LEO TAREHE 9 AGOSTI 2026

1. UTANGULIZI

Ndugu Waandishi wa Habari, Mtakumbuka kuwa Jumuiya ya Madola (The Commonwealth) imetoa maazimio yake kuhusiana na hali ya kisiasa nchini Tanzania baada ya uchaguzi batili uliopelekea matukio ya machafuko na mauaji ya Oktoba 2025 yaliyosababisha vifo vya watanzania wenzetu wasio na hatia zaidi ya 518 na majeruhi zaidi ya 2,390.

Nikiri wazi kuwa mimi **Luhaga Joelson Mpina** niliyekuwa Mgombea Urais wa Tanzania kupitia Chama cha ACT Wazalendo ni mmoja wa waliofika mbele ya Tume ya Mjumbe Maalum wa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola, **Mheshimiwa Dkt. Lazarus Mc Carthy Chakwera,** Rais Mstaafu wa Malawi mnamo tarehe 16 Aprili 2026 ambapo mazungumzo hayo yalichukua muda wa zaidi ya saa 3 wakati wa kuwasilisha maoni na mapendezo yangu yenye **Kurasa 70** kwenye tume hiyo.

2. RIPOTI NA MAAZIMIO YA JUMUIYA YA MADOLA

Baada ya kupitia Ripoti na maazimio ya Jumuiya ya Madola (The Commonwealth) yaliyotolewa tarehe 10 Julai 2026, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Jumuiya ya Madola kwa hatua

hiyo mzuri. Aidha shukrani za pekee zimwendee Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola **Mheshimiwa Shirley Ayorkor Botchwey.**

Pia natoa shukrani na pongezi nyingi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Chakwera kwa kazi mzuri aliyofanya ya kuchunguza na kujumuisha mapendekezo na maoni yetu kuhusiana na uchaguzi batili uliosababisha machafuko na mauaji ya wananchi wasio na hatia Oktoba 2025. Maoni na mapendekezo tuliyoyatoa yamefanyiwa kazi kwa kiwango kikubwa. **Asante sana.**

Aidha Jumuiya ya Madola imetoa maazimio manne (4) na ratiba ya utekelezaji wa maazimio hayo, kwa ujumla maazimio hayo ni mazuri sana na yatarejesha amani na utulivu nchini endapo yatatekelezwa kikamilifu.

Katika kutafakari maazimio 4 ya Jumuiya ya Madola ni muhimu wananchi kushinikiza utekelezaji wa maazimio haya lakini pia Jumuiya ya Madola kufuatilia kwa karibu hatua kwa hatua za utekelezaji wa maazimio yake kwani kuna wasiwasi mkubwa mtawala akapuuza maazimio hayo kama anavyofanya katika maeneo mengi. Pamoja na maazimio manne (4) ya Jumuiya ya Madola pia nimetoa Maoni na mapendekezo ya namna bora ya kutekeleza mapendekezo hayo kama ifuatavyo:-

(i) **Azimio Namba 1,** Ndani ya siku 30 kutatua suala la kuzuiliwa kwa Tundu Lissu kupitia njia ya kisiasa na kisheria pamoja na kuwaachia wanaoshikiliwa kwa kutumia haki zao za msingi kwa amani.

Mchakato wa kisheria ukamilike haraka ndani ya siku 30 zilizotolewa na Jumuiya ya Madola ili Tundu Antipas

Lissu aachiliwe huru baada ya kuonewa na kuteswa kwa muda mrefu bila sababu za msingi. Ni dhahiri kuwa alikamatwa na kufunguliwa kesi ya uongo ya uhaini ili kumdhibiti asigombee nafasi ya Rais katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Hata hivyo DPP amekuwa akizua mabishano yasiyo na msingi wa kisheria ikiwamo kuweka mapingamizi (POs) katika mashauri mbalimbali, mfano katika Kesi ya Uhaini ya Tundu Lissu, DPP aliwasilisha notisi ya nyongeza ya ushahidi (Notice of Substance of Evidence) chini ya Kifungu cha 308 cha Sheria ya mwenendo wa makosa ya Jinai (CPA) jambo ambalo lilikataliwa na Mahakama Kuu tarehe 24 Februari 2026 lakini Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) hakuridhika aliwasilisha maombi ya marejeo katika Mahakama ya Rufani kupinga uamuzi wa Mahakama Kuu ambapo mnamo tarehe 30 Julai 2026 Mahakama ya Rufaa chini ya jopo la Majaji watatu wakiongozwa na Mheshimiwa Jaji Mwarija wametupilia mbali madai ya DPP ya marejeo na kuuthibitishia umma uamuzi wa Mahakama Kuu ya Tanzania ulikuwa sahihi.

Huu ni uthibitisho kuwa DPP amekuwa akipoteza muda wa Mahakama na kurefusha muda wa kusikiliza mashauri ili kuwakomoa wakosoaji wa Serikali hususan kwa mashtaka ambayo hayana dhamana.

Wananchi wengi wanaendelea kukamatwa na kubambikizwa kesi za ugaidi na uhaini na kusota kwa muda mrefu katika mahabusu katika vituo vya Polisi na magerezani.

Mfano wa hivi karibuni ni tukio la Mwanachama wa CCM kutoka Wilaya ya Kwimba Mwanza, Ndugu **Devidlevi Nestory Nkindikwa Maarufu 'Kijana Mzalendo'** aliyepinga uteuzi wa Samia Suluhu Hassan wa kugombea urais ndani ya Chama cha Mapinduzi kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, alitekwa na kukaa kwenye gari kwa zaidi ya siku 3 bila maji wala chakula na baadaye kutelekezwa katika Vituo vya Polisi Oysterbay Dar es Salaam na Kibaha Mkoa Pwani kwa zaidi ya siku 45 sasa anasota mahabusu tangu alipotekwa Mnamo Juni 25, 2026 bila kupata haki ya dhamana, msaada wa kisheria wala kufikishwa Mahakamani huku makosa ya kukamatwa kwake yakiwa hayajawekwa wazi hadi sasa. Hata taarifa ziliporipotiwa kuhusu kutekwa kwake Jeshi la Polisi limekaa kimya hadi leo.

Pia **Mchungaji Dkt. Godfrey Malisa** aliyepinga uteuzi wa Samia kuwa mgombea kupitia CCM katika Mahakama Kuu ya Tanzania na baadaye Mahakama ya Rufaa naye alitekwa na watu wasiojulikana baadaye alifikishwa mahakamani kwa makosa ya uhaini na kushikiliwa gerezani kwa zaidi ya miezi 6 hadi kesi yake ilipofutwa na mahakama Mei, 2026 na wengine wengi huku akina Balozi Hamprey Polepole, Mdude Nyagali,

Deus Soka, Dioniz Kipanya na wengine wengi hawajulikani walipo hadi sasa. Tume ya Jaji Chande iliripoti kupotezwa kwa watu **758** katika kipindi cha miaka 3 kabla ya uchaguzi na kati yao **245** hawajulikani waliko hadi sasa.

Pamoja na wito wa kutaka wananchi wanaoshikiliwa waachiliwe huru mara moja lakini pia Serikali inapaswa kuwalipa fidia kwa unyama iliyowatendea wananchi hao.

(ii) **Azimio Namba 2,** Ndani ya siku 60, kurejesha kikamilifu upatikanaji wa majukwaa ya kidigitali na kusitisha vitisho dhidi ya vyombo vya habari na watetezi wa uhuru wa kujieleza.

Suala la Uhuru wa kutoa maoni na kujieleza ni jambo la Kikatiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Serikali ya awamu ya 6 imekuwa ikiwageuza wakosoaji na wachambuzi kuwa magaidi na hivyo kuwakamata na kuwashikilia mahabusu kwa muda mrefu. Mfano ni tukio la kukamatwa na kushtakiwa kwa makosa ya ugaid kwa **Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma 'UDOM', Dkt. Melkisedek Kitunzi Kaijage** akidaiwa kuhamasisha maandamano ya tarehe 7 Julai 2026, Dkt. Kaijage anatuhumiwa kutenda kosa hilo akiwa darasani wakati akifundisha wanafunzi wake. Jambo ambalo linaleta sintofahamu kubwa.

Pia Wanafunzi 18 wa Vyuo Vikuu vya IFM, CBE, UDSM, DMI, NIT, MNMA na KU wakiongozwa na **Kijana Frank Benjamin Kayamba** walikamatwa na kufikishwa Mahakamani Juni 12 2026 na kufunguliwa mashtaka 47 yakiwemo kujipatia mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) kwa njia ya udanganyifu ambapo Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu iliwaachilia huru wanafunzi hao tarehe 29 Julai 2026 baada ya kukubaliana na hoja ya utetezi kwamba hati ya mashtaka ilifunguliwa kimakosa na DPP na bila kufuata Sheria, lakini baadaye walikamatwa tena na Serikali.

Tarehe 23 Julai 2026 watu 23 mkoani Mwanza walikamatwa na kufikishwa Mahakamani kwa makosa ya ugaidi ambapo hati ya Mashtaka ilisainiwa na DPP mwenyewe, **Ndugu Sylvester Antony Mwakitalu**. Wakati hayo yakifanyika Waziri wa Mambo ya Ndani, **Patrobas Katambi** mnamo tarehe 29 Julai 2026 alitoa tamko la kukanusha kwamba nchini Tanzania hakuna ugaidi. Hizi ni Kauli na matendo ya Serikali moja ambao ni uthibitisho kuwa wananchi wamekuwa wakibambikiwa kesi ili kuwanyamazisha dhidi ya maovu yanayofanywa na Serikali.

Pia itakumbukwa baada ya machafuko ya Oktoba 2025 watu zaidi ya 1651 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani kwa makosa ya uhaini na baadaye kuachiliwa huru kwa kile kilichoitwa msamaha wa Rais.

Swali kubwa la kujiuliza kwanini kwenye nchi yetu watu wanyamazishwe, kwanini igeuzwe kuhoji na kukosoa Serikali iwe ni makosa ya uhaini na ugaidi, hii nguvu kubwa inayotumika kunyamazisha wananchi inalenga kuficha nini? Azimio hili utekelezaji wake ni mgumu bila kutatua chanzo cha tatizo.

(iii) **Azimio Namba 3,** Ndani ya siku 90 kuitisha jukwaa shirikishi lenye usimamizi huru litakalojadili mageuzi ya mfumo wa uchaguzi, ushindani wa kisiasa, masuala ya waliokamatwa na uwajibikaji.

Azimio hili linahitaji usimamizi wa karibu kutoka Jumuiya ya Madola ili liweze kutekelezwa, kwani hali ya kisiasa ni tete sana nchini mwetu kwa sasa. Mfano mtakumbuka tarehe 30 Julai 2026 mtawala alikutana na Viongozi wa Vyama vya Siasa Ikulu Dar es Salaam na kudai kuwa Vyama vyote vya Siasa wako vizuri isipokuwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ambacho alidai kuwa wanaendelea kupokea misukumo yake na matakwa yake.

Chama cha Demokrasia na Maendeleo mnamo tarehe 3 Agosti 2026 kimetoa taarifa kwa umma kuwa hakijawahi kukutana kwa siri wala kwa kificho na Chama Cha Mapinduzi kwa mazungumzo ya aina yoyote na kwamba msimamo wao unabaki uleule unaotokana na maazimio ya vikao vya Kamati Kuu ya CHADEMA bila ukweli, haki na Uwajibikaji hakuna maridhiano yoyote yatakayofanyika.

Pia msimamo wa Chama cha ACT Wazalendo umewekwa bayana kupitia Tamko la Chama la tarehe 9 Novemba 2025 na Maazimio ya Vikao vya Kamati Kuu vya Tarehe 18 Januari 2026 na tarehe 3 Mei 2026 ambavyo vyote vilisisitiza kuwa hakuna maridhiano bila **Ukweli, Haki na Uwajibikaji** na hadi sasa hakuna kikao kingine cha Chama kilichokutana kutengua msimamo huo.

Pia nikiwa Mgombea wa nafasi ya Rais niliyeenguliwa kwa hila na mabavu kugombea katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 kupitia Chama cha ACT Wazalendo kesi yangu bado iko mahakamani na sina mpango wa kuiondoa hadi isikilizwe na kuamuliwa. Kesi ya Tundu Lissu bado inaendelea mahakamani hivyo hayo maridhiano anayodai mtawala amefanya na nani?

Nilimsikia akisema utawala wake unatokana na Chama chake kushindwa uchaguzi, ukweli ni kwamba hakushinda katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 ila alijiweka madarakani kwa mabavu, wagombea wa nafasi ya Rais wa ACT Wazalendo na CHADEMA walizuiliwa kugombea kwa hila, Uchaguzi ulisimamiwa na Tume batili, matokeo batili na Viongozi wote Rais, Wabunge na Madiwani waliotangazwa ni batili na hawana ridhaa ya wananchi.

(iv) **Azimio Namba 4,** Kuanzisha uchunguzi huru wa jinai kama ulivyopendekezwa na Tume ya Uchunguzi

ikiwamo kuweka utaratibu wa fidia kwa waathirika, vigezo vya kustahili, fedha na ratiba ya utekelezaji.

Ni vigumu kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Chande ambayo ripoti yake haijatolewa kwenye umma hadi leo lakini pia haiwezekani kuwa na tume juu ya tume kwenye jambo moja.

3. KUHUSU DHANA YA MARIDHIANO

Duniani kote ni utaratibu wa kawaida kufanya maridhiano ya makundi yanayohasimiana baada ya vita au machafuko (the Aftermath) ambapo hatua hiyo hufikiwa baada ya ukweli kuwekwa wazi, Haki na Uwajibikaji chini ya msimamizi huru asiyefungamana na upande wowote (Neutral/Impartial Person). Pia hadidu za rejea hukubalika na pande zote kabla ya uchunguzi kuanza.

Maridhiano baada ya matukio ya machafuko na mauaji ya Oktoba 2025 hapa nchini kwetu yanaweza kuwa magumu kufikiwa pamoja na kupigiwa kampeni za kila aina na mtawala na washirika wake kwani Serikali na Mtawala hawapo tayari kuweka ukweli, uwazi, haki na uwajibikaji kuhusiana na machafuko ya Oktoba 2025 na badala yake inafanya propaganda na ulaghai wa kila aina. Mfano:-

(i) Mtawala aliunda Tume isiyo huru ya kuchunguza matukio ya Oktoba 2025 na baadae akaficha Ripoti hiyo isisomwe na mtu yoyote zaidi yake akidai ni mali yake. Hivyo hakuna chombo kingine kitakachoweza kufahamu ukweli na uwazi, haki na Uwajibikaji kupitia ripoti hiyo isipokuwa yeye tu.

(ii) Pia Tarehe 7 Agosti 2026 amezindua Tume nyingine ya kuchunguza mambo ya Jinai huku akitoa hadidu za rejea kuwa tume hiyo iende ikachunguze kwa undani na kuwafahamu waliotoa fedha kufadhili maandamano jambo ambalo amekuwa akilirudia mara kwa mara na inajidhihirisha wazi kuwa analenga kuwakomoa baadhi ya watu anaowachukia binafsi na kwa maslahi binafsi huku akitapanya fedha za umma. Pia tume hizo zimekuwa zikipewa muda mrefu kukamilisha kazi zake ili kuwapotezea muda wananchi na Jumuiya za Kimataifa.

(iii) Tume ya Uchunguzi wa Kijinai iliteuliwa na mtawala tangu tarehe 18 Mei 2026 ikiwa na wajumbe 4, lakini tarehe 7 Agosti 2026 akizindua tume hiyo akatangaza wajumbe wawili wapya kutoka Namibia na Uganda jambo ambalo linaleta mkanganyiko mkubwa namna alivyowapata wajumbe hao.

(iv) Serikali kuzidisha ubabe na vitendo vya dhuluma, uonevu na unyanyasaji kwa wananchi vimeshamiri ikiwemo kubambikwa kesi za uhaini na ugaidi kila uchao, kutekwa, kunyang'anywa mashamba na mifugo, kupoteza masoko ya mazao, huduma za Kijamii na Kiuchumi kudorora.

(v) Mtawala huku akijiua kuwa yeye ni mtuhumiwa namba moja wa machafuko na mauaji ya Oktoba 2025 ameanza kuitisha vikao vya maridhiano na makundi na Vyama vya Siasa. Msimamo wa Umma wa Tanzania,

Asasi za Kiraia, Viongozi wa dini, TLS, Wanaharakati na wanazuoni wanataka ukweli na uwazi, haki na Uwajibikaji kabla ya hatua ya maridhiano. Hivyo maridhiano yoyote yanayoendelea hivi sasa nchini ni kiini macho na ni maridhiano feki.

(vi) Mtawala ametangaza wanaharakati ni magaidi na baada ya siku chache tukaanza kushuhudia wakosoaji wa Serikali wakikamatwa na kufunguliwa kesi za ugaidi, lakini tangu kesi hizo zianze kufunguliwa na DPP serikali haijashinda kesi hata moja, huu ni ushahidi kuwa kesi hizo ni za uongo na zinafunguliwa kwa lengo la kuwakomoa, kuwatisha na kuwanyamazisha wananchi wanaopinga maovu yanayofanywa na Serikali.

Kutokana na kukosekana kwa dhamira ya dhati ya kisiasa ya Mtawala, Jumuiya ya Kimataifa ikiongozwa na Jumuiya ya Madola, AU na UN, viongoze muelekeo mpya wa kuwepo kwa Tume ya kupata ukweli, Haki na Maridhiano itakayo ongozwa na watu huru mashuhuri wa ndani na nje ya nchi mfano maridhiano yaliyofanyika nchini Afrika ya Kusini mwaka 1995 ambapo ulikuwa ni mchakato wa kuleta pamoja makabila na watu wa rangi mbalimbali baada ya kumalizika kwa mfumo wa ubaguzi wa rangi (Apartheid Regime) mwaka 1994. Mchakato ambao uliongozwa na Tume ya Ukweli na Maridhiano (TRC) chini ya **Askofu Desmond Tutu.**

Tume hiyo ya ukweli na maridhiano ilianzishwa mwaka 1995 kupitia Sheria ya Bunge na ilisikiliza ushahidi kutoka kwa waathiriwa na wakosaji wa ukiukwaji wa haki za binadamu ambapo ilitoa nafasi ya msamaha kwa waliofanya makosa ya

kisiasa kama walisema ukweli wote ambapo lengo lilikuwa kujenga taifa jipya lenye amani bila kulipiza kisasi.

Mfano mwingine ni nchi ya Kenya, baada ya machafuko na mauaji ya ghasia za uchaguzi mwaka 2007 yalianzishwa maridhiano kupitia Mkataba wa Pwani (National Dialogue and Reconciliation uliotiwa saini mwezi Februari 2008 ukisimamiwa na jopo la watu mashuhuri wa Afrika (Panel of Eminent African Personalities) chini ya Umoja wa Afrika (AU), likiongozwa na Katibu Mkuu wa zamani wa Umoja wa Mataifa, **Kofi Annan** ambapo wajumbe wengine wa jopo hilo walikuwa ni **Benjamin Mkapa**, Rais Mstaafu wa Tanzania na **Graca Machel**, Mwanaharakati wa haki za Binadamu na Mke wa zamani wa Nelson Mandela na Samora Machel.

Tume hiyo ilifanikiwa kuwakutanisha Rais **Mwai Kibaki** na Kiongozi wa upinzani, **Raila Odinga** kusaini mkataba wa kugawanya madaraka uliofanya Mwai Kibaki kuwa Rais na kuunda nafasi ya Waziri Mkuu iliyoshikiliwa na Raila Odinga.

Pia Mkataba huo ulioongozwa na jopo hilo uliunda Tume ya Uchunguzi wa Machafuko (Tume ya Waki-CIPEV), Tume huru ya uchaguzi (IREC) na Tume ya ukweli, haki na maridhiano (TRJRC) ili kushughulikia misingi ya migogoro hiyo na kuleta mabadiliko ya Kikatiba ambapo hatimaye mwaka 2010 nchi ya Kenya ikapata Katiba Mpya.

Kwa mazingira yaliyopo nchini mwetu ni vigumu sana kufikia maridhiano kwa kuwa mtawala ameatamia mambo yote na kujigeuza yeye kuwa msuluhishi na mpatanishi wa machafuko ya

Oktoba 2025, lakini pia ni vigumu zaidi kutekeleza maazimio ya jumuiya za kimataifa kwa wakati na kwa kiwango cha kuridhisha.

4. TUME YA KUCHUNGUZA MAMBO YA KIJINAI

Baada ya kuwasilisha Muhtasari wa Ripoti ya Tume ya Rais ya kuchunguza matukio ya ghasia na uvunjifu wa amani yaliyotokea kabla, wakati na baada ya uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, 2025 ilipendekezwa kuundwa Tume ya Kijinai tarehe 23 Aprili 2026.

Tume ya Rais ya uchunguzi wa kijinai ilitangazwa na Mtawala tarehe 18 Mei 2026 na kuzinduliwa tarehe 7 Agosti 2026, tume ambayo ilipingwa na watanzania wengi kwani haiwezekani kuunda Tume 2 kwa madhila yanayotokana na tukio moja na kwamba kufanya hivyo ni kuwapotezea muda wananchi, kukwepa uwajibikaji, kufuja fedha za umma na kukwepa mchakato wa Mahakama ya Kimataifa ya uhalifu (ICC). Baadhi ya Wanaharakati nchini Tanzania wakiongozwa na **Bubelwa Buberwa** na **Joseph Mabugo** walifungua kesi Mahakama Kuu kupinga tume hiyo.

Jambo lingine la kushangaza ni nchi ya Namibia na Uganda kukubali kutumika kuja kuhalalisha matendo ya kikatili yaliyofanywa na Serikali ya Tanzania Oktoba 2025, Kwa kuwaruhusu Naibu Jaji Mkuu wa Namibia, **Mheshimiwa Petrus Tilainge Damaseb** na Jaji wa Mahakama ya Rufani Uganda, **Mheshimiwa Barishaki Cheborion** kuwa katika Tume ya Kijinai baada ya kuteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kinyume na Mkataba wa Afrika (The African Charter on Democracy, Election and Governance of 2007) ambayo imejengwa katika kanuni kuu 4, Uzingativu wa Katiba, uchaguzi bora, haki za binadamu na uwazi na uwajibiaji.

(i) Uchaguzi wa Tanzania haukuwa huru wala haki na waangalizi kutoka AU, SADC na Jumuiya za Kimataifa walikiri kuwa uchaguzi wa mwaka 2025 haukukidhi viwango vya Demokrasia, leo Majaji hao tena wabobevu wa Sheria wamekubali vipi kuteuliwa na kuapishwa na Rais ambaye hakuchaguliwa kidemokrasia, hii ni kinyume na mkataba wa Afrika (Unconstitutional and against Electoral Standards).

(ii) Majaji hawa wamekubali vipi kuteuliwa na kuapishwa na mtuhumiwa tena aliye nje ya mamlaka yao kisheria (Geographic jurisdiction), utaratibu uliotumika kuwateua hauko wazi na haukutangazwa nchini kwani uteuzi wao ungeweza kufanywa na AU, SADC na EAC na sio mtawala wa Tanzania wala Tume ya Mahakama ya Namibia na Uganda.

(iii) Tume ya Kijinai ilitokana na mapendekezo ya Tume ya Jaji Chande ambayo ripoti yake aliificha Rais na kuwa siri yake pekee, nchi nzima ya Tanzania hadi sasa haijui kilichomo katika ripoti hiyo imebaki kuwa siri ya mtawala, hadidu za rejea za tume hiyo hazijaelezwa hadharani imewezekana vipi Wanasheria wabobevu hawa wakubali kushiriki kwenye jambo ambalo ni siri ya mtu mmoja ndani ya nchi kitendo ambacho kina kinzana na dhana ya uwazi na uwajibikaji iliyowekwa katika mkataba wa Afrika (Transparency and Accountability)

(iv) Majaji hao wamekubali kupokea maelekezo hadharani ya namna ya kwenda kuisafisha Serikali pale walipoambiwa waende wakatafute nani hasa waliochochea, waliohusika na waliotoa fedha ili yale mambo yatokee ndani ya nchi na sio kwenda kuchunguza nani hasa aliyehusika kutoa amri na kutekeleza mauaji ya kikatili ya watu zaidi ya 518 wasio na hatia na kusababisha majeruhi ya watu zaidi ya 2,390, agizo hili lina mgongano mkubwa wa maslahi (Conflict of Interest) na linaingilia moja kwa moja uhuru wa Tume kufanya uchunguzi (Impartiality of the Commission)

(v) Tume ya Jaji Chande na Tume ya Jaji Lila sio huru na zimeundwa bila kuzingatia Kanuni, miongozo na taratibu za usuluhishi wa migogoro (Conflict Resolution Strategies and Guidelines) na hivyo haikutegemewa Majaji kutoka Namibia na Uganda kukubali uteuzi.

Aidha nichukue nafasi hii kuvipongeza Vyama vya Siasa nchini Namibia vya **Affirmative Repositioning (AR)** na Chama cha **Independent Patriots for Change (IPC)** kwa kumtaka Naibu Jaji Mkuu wa Namibia, **Mheshimiwa Petrus Damaseb** kukataa uteuzi huo kwani utaratibu uliotumika kumteua ni wa kisiasa na haueleweki, kuapishwa bila kuziona hadidu za rejea na kwamba Serikali ya Namibia haijaweka wazi namna ilivyoshughulikia madai ya ukiukwaji wa haki za binadamu na uminywaji wa demokrasia nchini Tanzania tangu umalizike uchaguzi wa Oktoba 2025, hivyo kushiriki kwenye tume yenye dosari nyingi kiasi hicho kutashusha

hadhi yake binafsi Mheshimiwa Damaseb na itachafua taswira nzima ya Mahakama ya Namibia kimataifa.

5. MAMBO NILIYOIELEZA TUME YA RAIS CHAKWERA

Ndugu Waandishi wa Habari, nilifanikiwa kukutana na Tume ya Chakwera ambapo mazungumzo yetu yalichukua zaidi ya saa 3 na kisha kukabidhi ripoti yenye kurasa 70 iliyosheheni nyaraka za ushahidi wa kila aina baadhi ya mambo hayo niliyomueleza kwa muhtsari ni kama ifuatavyo:-

(i) Ndugu Samia Suluhu Hassan ashauriwe kujiuzulu nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuliponya taifa na kuanza upya.

(ii) Uchaguzi haukuwa huru na haki jambo ambalo pia lilithibitishwa na watazamaji wa kimataifa wa SADC na AU, uchaguzi ulikuwa batili na ulisimamiwa na Tume batili hivyo Viongozi wote Rais, Wabunge na Madiwani waliotangazwa ni BATILI.

(iii) Vyama vikuu vya upinzani CHADEMA na ACT Wazalendo hususan kwa nafasi ya Rais kwa upande wa Tanzania bara vilizuiliwa kwa mabavu kushiriki uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ambapo Serikali kupitia Msajili wa Vyama vya Siasa (RPP), INEC, AG na Mahakama vilitumika kuwadhibiti na kuwaengua wagombea wa vyama vya upinzani kwa mabavu ambapo mimi **Luhaga Joelson Mpina,** Mgombea Urais kupitia Chama cha ACT Wazalendo niliienguliwa na INEC kwa mabavu na kinyume cha Sheria na Katiba ya Nchi.

Tume ya Uchaguzi iliniengua kwa kutumia taarifa za uongo za Msajili wa Vyama vya Siasa aliyedai kuwa mimi nilijiunga na ACT Wazalendo tarehe 5/8/2025 wakati ukweli mimi nilijiunga tangu tarehe 29/7/2025 na hakuna kifungu cha Katiba wala kanuni yoyote ndani ya Chama cha ACT Wazalendo iliyokuwa imekiukwa.

Pia Mwenyekiti wa CHADEMA, **Ndg. Tundu Antipas Lissu** wakati nchi inakaribia kuanza mchakato wa uchaguzi Aprili 2025 alikamatwa na kushtakiwa kwa tuhuma za uongo za uhaini na Chama chake cha CHADEMA kufungiwa kushiriki shughuli za siasa. Lengo na madhumuni likiwa ni kumwezesha mgombea wa CCM **Ndugu Samia Suluhu Hassan** kupita bila kupingwa.

(iv) Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 ulisimamiwa na Tume batili na matokeo yaliyotangazwa yalikuwa batili na yana udanganyifu mkubwa ndiyo maana Tume batili ya uchaguzi imeshindwa kutangaza matokeo hayo kwenye gazeti la Serikali hadi leo. Pia mtawala alikwenda kuapishwa kwenye Kambi ya Jeshi (Military Barracks) kule Dodoma, huku wabunge na madiwani wengi wakikabidhiwa hati za ushindi makao makuu ya Kata na Wilaya badala ya kutangaza matokeo hadharani.

(v) Maandamano ya Oktoba 2025 yalisababishwa na kukithiri kwa vitendo vya wizi, rushwa, ufisadi na ubadhirifu mkubwa wa fedha na raslimali za umma, pamoja na kuminywa kwa demokrasia na vitendo vya watu kutekwa, kupotea na kuuawa. Hivyo wananchi

walipomuona mtawala amejiteua hawakuwa na njia nyingine zaidi ya kuandamana kudai nchi yao.

(vi) Waandamanaji wengi waliuawa na kujeruhiwa kwa makusudi na kwa chuki ya Serikali ya CCM na kwamba walikuwa na haki kisheria na kikatiba kitaifa na kimataifa.

(vii) Mahakama ya Tanzania haiko huru na inapokea maelekezo kutoka kwa watendaji na Viongozi wa Serikali. Aidha kuna mahitaji makubwa ya mabadiliko ya sheria za uchaguzi na kutungwa kwa Katiba mpya.

(viii) Tume ya Uchunguzi ya matukio ya Oktoba 2025 iliyoundwa na Mtawala sio huru na haitarajiwi kuleta matokeo yanayoaminika na imechelewa kutoa ripoti yake bila sababu za msingi.

(ix) Jumuiya za Kikanda za Afrika za EAC, SADC na AU ziko kimya na badala yake Jumuiya ya Madola (The Commonwealth), EU, Marekani (USA) na UN ndizo zinazofuatilia machafuko ya kisiasa nchini Tanzania.

6. MAONI NA MAPENDEKEZO NILIYOYATOA KWA TUME YA DKT. CHAKWERA

Nilitoa Maoni na mapendekezo kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

(i) Kuundwa Tume Huru ya Uchunguzi itakayo ongozwa na Jumuiya ya Madola au taasisi yoyote ya kimataifa ambayo Tanzania ni mwanachama haraka iwezekanavyo.

(ii) Waathirika na familia wanahitaji fidia na kuona uwajibikaji na hatua stahiki za kuponya majeraha waliyopata.

(iii) Kufumua sheria za uchaguzi na kutungwa kwa Katiba mpya ambayo itahakikisha kwamba Tume ya Uchaguzi na mfumo mzima wa uchaguzi unakuwa huru na wenye uwazi ili kukidhi mahitaji ya mfumo wa Vyama vingi nchini.

(iv) Kufuta matokeo ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 na kuitisha uchaguzi mpya haraka iwezekanavyo.

(v) Kesi zote zinazohusu uchaguzi wa mwaka 2025 zisikilizwe na kuamuliwa zikiwemo nilizofungua mimi binafsi (Luhaga Joelson Mpina) na chama cha ACT Wazalendo dhidi ya INEC na AG na Kesi ya Luhaga Joelson Mpina na Chama cha ACT Wazalendo dhidi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na AG, ambazo zimepakiwa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa.

(vi) Wafungwa wote wa kisiasa na waliotekwa wakiwemo mh Tundu Lissu, Balozi Humphrey Polepole na Mchungaji Dkt. Godfrey Malisa na wanaharakati wengine waachiwe huru bila masharti yoyote.

(vii) Viongozi mashuhuri hususan wastaafu wenye ushawishi na heshima Barani Afrika washinikize jumuiya za kikanda na Umoja wa Afrika kuunda chombo cha Wazee ambacho kitakuwa rufaa ya migogoro na machafuko ya kisiasa Barani Afrika.

(viii) Umoja wa Afrika (AU) na Jumuiya za kikanda (SADC, EAC) waache upendeleo katika utoaji adhabu kwa kusitisha kwa muda uanachama wa nchi zinazopinduliwa kijeshi (military coup) kwa kutoa adhabu kama hiyo kwa viongozi wa Kiraia wanaopoka madaraka kwa kuiba uchaguzi, kutumia mabavu ya vyombo vya dola na kubadili Katiba ili kubaki madarakani maisha kinyume na matakwa ya kidemokrasia na utawala bora.

Aidha nilikabidhi taarifa kwa maandishi ambayo iliambatanishwa na vipande vya video, vivuli vya nyaraka muhimu na bangokitita la kesi ya rufaa yenye kurasa 448 ambayo kwa pamoja niliwasilisha kwa Dkt. Chakwera na ujumbe wake tulipokutana Dar es Salaam tarehe 16 Aprili 2026.

7. HITIMISHO

Ndugu Waandishi wa Habari, kumekuwa na kupuuzwa kwa miito mbalimbali ya Jumuiya za Kimataifa kuhusu matukio ya kabla, wakati na baada ya uchaguzi Mkuu wa tarehe 29 Oktoba 2025 ambapo mtawala mara kwa mara amekuwa akinukuliwa akisema asiingiliwe na jumuiya hizo na kuhoji **Who Are You?**

Mpaka sasa hakuna nia ya dhati na utashi wa kisiasa wa kutekeleza Maazimio ya Jumuiya za Kimataifa likiwemo Bunge la Ulaya (EU Parliament), Bunge la Marekani (Congress) na Jumuiya ya Madola kwani serikali, licha ya kupewa maonyo mbalimbali, serikali imezidisha zaidi dhuluma na uonevu kwa wananchi ikiwemo ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu, wananchi

kukamatwa na kufunguliwa kesi za kubambikwa za uhaini na ugaidi.

Aidha tangu machafuko ya Oktoba 2025 yaliyosababisha mauaji ya watu wasio na hatia zaidi ya 518 na majeruhi zaidi ya 2,390 na kuminywa kwa demokrasia ya Vyama vingi, nchi za Jumuiya za Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) hazijajishughulisha na mkwamo wa kisiasa uliolikumba taifa letu la Tanzania jambo ambalo ni la kushangaza na sio kawaida kwani tunakumbuka yalipotokea machafuko ya uchaguzi nchini Kenya mwaka 2007 AU ilipeleka Tume ya usuluhishi ambayo ilifanya kazi nzuri na muafaka ukapatikana.

Kwa kuwa Jumuiya za Afrika zimejiweka kando na Serikali ya Tanzania kukosa dhamira ya dhati ya kuitoa nchi yetu kwenye mkwamo natoa wito kwa Jumuiya za Kimataifa kuingilia kati na kufuatilia hatua kwa hatua utekelezaji wa maazimio inayoyatoa kuhusu Tanzania. Aidha kwa hali inayoendelea nchi yetu inaenda kutengwa, kuwekewa vikwazo au kufukuzwa uanachama katika Jumuiya za Kimataifa.

Taifa letu ni changa na kwamba ustawi wake unategemea ushirikiano na nchi nyingine ikiwemo upatikanaji wa mikopo, dawa za aina zote, masoko ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini, pembejeo, nguo, matibabu, biashara, ushirikiano wa kitaaluma, masomo, kidiplomasia, wawekezaji na watalii nk.

Baadhi ya nchi za Afrika zilizowahi kutengwa, kuwekewa vikwazo na kusimamishwa uanachama wa Jumuiya ya Madola, Mfano nchi

ya Zimbabwe, CMAG iliisimamisha uanachama Zimbabwe tangu Machi 2002 ni miaka 24 iliyopita kufuatia ghasia za uchaguzi wa urais uliokuwa na ushindani mkubwa baina ya **Robert Mugabe** wa Chama cha ZANU PF na **Morgan Tsvangirai** wa Chama cha Movement for Democratic Change (MDC). Kutengwa kwa nchi ya Zimbabwe na Jumuiya ya Madola kumepelekea wananchi wa taifa hilo kupata mateso na matatizo makubwa hadi leo.

Tayari nchi yetu imeanza kuonja madhila makubwa ya kuwekewa vikwazo na Jumuiya za Kimataifa licha ya Serikali kueleza kuwa wamepeleka barua 25 za kujitetea Duniani, Marekani ilipitisha Azimio la kisheria la Maseneta wake wawili ambao ni **Ted Cruz** wa Chama cha Republican na **Jeanne Shaheen** wa Chama cha Democrat ya kuionya na baadae kuiwekea vikwazo Tanzania. Kwa sasa Marekani imeweka vikwazo kwa watanzania kupata Visa na kusababisha usumbufu mkubwa hususan kwa wanafunzi, wagonjwa wanaosoma na kutibiwa Marekani lakini pia wafanyabiashara na wawekezaji.

Pia Bunge la Jumuiya ya Umoja wa Ulaya limepitisha Azimio la kuinyima Tanzania misaada ya EURO Milioni 156 sawa na Tsh Bilioni 440, Jumuiya ya Madola (The Commonwealth) imetoa maazimio 4 na ratiba ya utekelezaji na baada ya hapo itachukua hatua ikiwemo kuweka vikwazo vya kiuchumi.

Matamko ya mtawala kuhusu msimamo wa Jumuiya za Kimataifa kuwa jumuiya hizo zinaingilia uhuru wa nchi ni kuchochea uhasama na mgogoro wa kidiplomasia kimataifa kwani mikataba ya kimataifa iko wazi kuhusu Haki za Binadamu na Demokrasia ambayo Tanzania imeridhia (The United Nations Convenctional on

Civil and Political Rights of 1966, The Universal Declaration on Human Rights of 1948 nk)

Kwa muda mrefu Tanzania imekuwa mwanachama mtulivu na kisiwa cha amani katika Jumuiya za kimataifa wala haijawahi kujieleza, kuwekewa vikwazo wala kusimamishwa uanachama katika Jumuiya ya Madola na badala yake Tanzania imekuwa msuluhishi wa migogoro ya kisiasa katika mataifa mbalimbali na zaidi ya yote Tanzania imewahi kutoa hadi Katibu Mkuu wa Bunge la Jumuiya ya Madola,(Secretary General of The Commonwealth Parliamentary Association) **Dkt. William Ferdinand Shija** akiwa mwafrika wa kwanza kushika wadhifa huo kwenye taasisi hiyo muhimu. Pia imewahi kutoa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) **Dkt. Asha Rose Migiro**.

Watanzania tusikubali taifa letu kuingizwa kwenye mgogoro mkubwa wa kidiplomasia na Kiuchumi kwa ubabe wa watawala ambapo sababu za kufanya hivyo wanazijua wao. Abadan, Asilan tusikubali. Ni lazima kushinikiza Ukweli, Haki na Uwajibikaji.

8. MWISHO

Msimamizi huru (Mediator) atafutwe kwa uangalifu mkubwa na kwa wakati ili kulinusuru taifa letu na kurejesha amani, utulivu na demokrasia ya kweli nchini. Wapo watu mashuhuri na wenye uzoefu mkubwa katika utatuzi wa migogoro ya kisiasa sehemu mbalimbali Duniani kama **Mzee Thabo Mbeki, Abiy Ahmed, Dkt. Lazarus Chakwera, Mzee Olusegun Obasanjo** nk.

Pia ndani ya nchi yetu wako watu wanaoheshimika na kuaminika katika kusimamia haki kama **Mzee Jaji Joseph Sinde Warioba, Profesa Anna Tibaijuka, Mzee Juma Duni Haji (Babu**

Duni), Profesa Raymond Mosha, Profesa Issa Shivji, Dkt. Hellen Kijo Bisimba na Mzee Jenerali Twaha Ulimwengu.

Ndugu Waandishi wa Habari, natoa wito kwa Watanzania wote mlioko mijini na vijijini kuchukua hatua ya kushinikiza kwa Mtawala na Serikali yake kufanya yafuatayo:-

(i) Kutekeleza maazimio ya Jumuiya za Kimataifa ikiwemo Bunge la Ulaya, Bunge la Marekani na Jumuiya ya Madola, kwa wakati kabla ya nchi yetu haijatumbukia kwenye matatizo makubwa ikiwemo kutengwa, kuwekewa vikwazo katika shughuli za Kijamii na Kiuchumi au kufukuzwa uanachama.

(ii) Kuchukua hatua za kukomesha vitendo vya uvunjifu wa Sheria na Katiba ya Nchi unaofanywa kwa makusudi na Serikali ya awamu ya 6 (Unconstitutional and Lawlessness) na kupelekea kushamiri kwa vitendo vya Wizi, Rushwa, Ufisadi na ubadhirifu wa fedha na raslimali za umma. Matukio ya watu kutekwa, kupotezwa na kuuawa pamoja na kuminywa kwa demokrasia nchini. Kukomesha dhuluma na uonevu wa kila aina ulioshamiri kila pembe ya nchi na kuathiri zaidi wanyonge.

(iii) Kupatikana Katiba Mpya na kufumua Sheria zote za uchaguzi na kutungwa upya mapema kabla ya mwaka 2028.

(iv) Kufutwa kwa uchaguzi batili wa Oktoba 2025 na kuitishwa uchaguzi mpya ili kuwapa nafasi wananchi

kuchagua Viongozi wao wanaowataka katika ngazi ya Rais, Wabunge na Madiwani.

Pamoja na taarifa hii nimeambatisha ripoti yenye **Kurasa 70** ambayo niliwasilisha mbele Tume ya Dkt Chakwera kwa ajili ya rejea muhimu hasa katika kipindi hiki kigumu ambacho taifa letu linapitia.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

Luhaga Joelson Mpina

Aliyekuwa Mgombea wa Urais wa Tanzania kupitia Chama cha ACT Wazalendo Uchaguzi Mkuu 2025 na Naibu Waziri Waziri Mkuu Kivuli